

Washauri wa ADIS watakusikiliza na kuzungumza na wewe kuhusu:

- Maswali na matatizo yako,
- Usaidizi na msaada uliopo kwa ajiri yako.
- Marejeo kwa huduma zingine za msaada.

**Wakalimani wanapatikana bila malipo.**

ADIS ina wafanyakazi wenye uzoefu, washauri wenye utaalamu na hutoa huduma mbalimbali ikiwa ni pamoja na:

- Ushauri wa pombe na madawa ya kulevya kwa njia ya simu.
- Habari kuhusu pombe na madawa ya kulevya na mwili wako.
- Habari kuhusu huduma ya matibabu na msaada wa kidaktari wa pombe na madawa ya kulevya.

**Tafadhali pigia ADIS kama unahitaji habari na msaada.**

**ADIS – 9442 5000 au  
1800 198 024  
bure kwa wapigaji wa vijijini**

Email: [adis@health.wa.gov.au](mailto:adis@health.wa.gov.au)

Tovuti: [www.dao.health.wa.gov.au](http://www.dao.health.wa.gov.au)

Anwani: ADIS, PO Box 126, Mt Lawley, WA 6929

Fax: 9442 5020

Huduma ya ukalimani na Utafsiri 131450

Huduma ya Msaada ya Kitaifa 133677

(kwa wale wasiosikia au kutokusema).

## **HUDUMA YA HABARI Za Pombe Na Madawa Ya Kulevya**

**ALCOHOL AND DRUG INFORMATION SERVICE (ADIS)**

**Je una wasiwasi kuhusu pombe  
au madawa ya kulevya?**

**Je vinakusababishia matatizo?**

**Je unahitaji habari na msaada?**



Government of Western Australia  
Drug and Alcohol Office

**Piga simu:  
9442 5000 au 1800 198 024  
bure kwa wapigaji wa vijijini**

Kumbuka, wakati unafikiria kuhusu pombe na madawa ya kulevya, kuna aina nyingi za madawa ya kulevya kama vile bangi, heroin, amfetamin (kasi, barafu), dawa kutoka kwa daktari au duka la dawa, miraa, tumbaku, na zingine zinazoweza kusababisha matatizo.

### Haya ni baadhi ya maswali ya kukusaidia kuamua:

- Je kuna ndugu wa familia au marafiki ambao wameshalalamikia kutumia kwako pombe au madawa ya kulevya?
- Je, umewahi kutumia pombe au madawa ya kulevya kama kitu cha kuanzia asubuhi?
- Je, umewahi kutumia pombe au madawa ya kulevya kama kitu cha kukupitisha siku?
- Je, wewe au mtu mwingine amewahi kuumizwa kwa sababu ya pombe au madawa ya kulevya?
- Je, umewahi kuficha pombe au madawa ya kulevya kutoka kwa familia au rafiki, kwa sababu unaona kujidharau, aibu au hofu?
- Je, kutumia pombe au madawa ya kulevya kunaathiri maeneo mengine ya maisha yako, kwa mfano, mahusiano ya familia, kazi, marafiki, fedha, au afya?
- Je, umewahi kuishiwa fedha ys vitu unavyohitaji, kama vile chakula au kulipa bili yako, kwa sababu wewe alitumia fedha kwa ajili ya pombe au madawa ya kulevya?
- Je, umewahi kupatwa na matatizo ya kisheria au kuwa matatizoni na polisi kwa sababu ya pombe au madawa ya kulevya, kwa mfano kuendesha ukiwa emelewa, uzembe au makosa ya utumiaji madawa?

Kama umejibu ndiyo kwa swali lolote la haya basi inawezekana kuwa unahitaji kuzungumza na mtaalamu.

### Msaada ni kupiga simu tu kidogo

Kama unapenda kuzungumza na mtu, na kujadili njia za kupata msaada, unaweza kuita Huduma ya Habari za Pombe na Madawa ya Kulevya (ADIS).

Hii ni huduma ya bure na ya siri ambayo inapatikana kwa masaa 24 kwa siku, siku 7 kwa wiki. Hakuna mtu anayehitaji kujua kwamba umepiga kuomba msaada, ushauri, au usaidizi. **Habari zako hazitolewa kwa mtu mwingine yeyote ikiwa ni pamoja na polisi.**

